



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MKATABA WA MUDA MFUPI

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia Watanzania wenye sifa kuomba kazi za mkataba wa muda mfupi kwa Kada za TEHAMA na Kada ya Ununuzi na Ugavi kwa ajili ya uboreshaji wa Daftari la kudumu la Wapiga Kura.

1. KADA YA TEHAMA

(Nafasi 200- Dar es Salaam na nafasi 50- Dodoma)

A: Sifa za mwombaji kwa Kada ya TEHAMA

- i. Awe na cheti cha kidato cha nne na kuendelea, mwenye uzoefu wa kufanya kazi Tume itakuwa ni sifa ya ziada;
- ii. Awe na cheti cha shahada au stashahada au astashahada katika fani ya TEHAMA (ICT/IT), Electronics au Electrical inayotolewa na chuo kinachotambulika na Serikali au fani nyingine yoyote inayoendana na masuala ya TEHAMA au cheti cha kozi ya Kompyuta au mwenye ujuzi wa kompyuta;
- iii. Awe mwenye ujuzi wa kutumia Kompyuta na simu janja (Smartphone) pamoja na kufanya matengenezo madogo madogo ya vifaa hivyo;
- iv. Asiwe mwajiriwa katika Utumishi wa Umma;
- v. Asiwe ametiwa hatiania kwa makosa ya jinai ndani ya miaka mitano kabla ya kuomba ajira hii; na
- vi. Awe mwadilifu na mwaminifu.

B: Kazi na Majukumu:-

- i. Kuandaa vifaa vya uboreshaji ikiwa ni pamoja na kuviunganisha na kuvichaji;
- ii. Kuweka programu mbalimbali za TEHAMA;
- iii. Kuhakiki vifaa vyote vya TEHAMA vilivyopo ofisi za Tume;
- iv. Kutoa ushauri wa kiufundi kwa watendaji wa halmashauri wakati wa utekelezaji wa shughuli zinazosimamiwa na Tume;
- v. Kusaidiana na watumishi wa Tume katika kutoa mafunzo kwa watendaji wa halmashauri kuhusu matumizi ya TEHAMA;
- vi. Kufanya matengenezo kinga kwenye vifaa vya TEHAMA; na
- vii. Kutekeleza majukumu mengine atakayopangiwa na Msimamizi wa kazi wa sehemu husika.

2. KADA YA UNUNUZI NA UGAVI

(Nafasi 150- Dar es Salaam)

A: Sifa za Mwombaji kwa kada ya Ugavi na Ununuzi

- i. Awe na cheti cha kidato cha nne na kuendelea. Mwenye uzoefu wa kufanya kazi Tume itakuwa ni sifa ya ziada;
- ii. Awe na afya njema;
- iii. Awe na uwezo wa kufanya kazi katika mazingira yoyote;
- iv. Awe na uwezo wa kufanya kazi kwa muda wote na muda wa ziada;
- v. Mwenye cheti cha shahada au stashahada au astashahada ya masomo ya ununuzi na ugavi ni sifa ya ziada; na
- vi. Awe mwadilifu na mwaminifu.

B: Kazi na Majukumu:-

- i. Kuingiza taarifa za vifaa kwenye *store ledger*;
- ii. Kushiriki katika zoezi la kuhesabu vifaa (stock taking);
- iii. Kutunza vifaa katika maghala ya Tume;
- iv. Kuhakikisha usalama wa vifaa na maghala;
- v. Kupakia na kushusha vifaa;
- vi. Kufungasha vifaa mbalimbali;
- vii. Kupanga vifaa kwenye maghala;
- viii. Kufanya usafi kwenye maghala na;
- ix. Majukumu mengine atakayopangiwa na Msimamizi wake.

3. MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE

- i. Mwombaji awe Raia wa Tanzania na mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45;
- ii. Mwombaji aambatishe nakala ya vyeti vya Elimu ya Sekondari na Taaluma vinavyohitajika kulingana na kada husika kama ilivyofafanuliwa katika tangazo hili;
- iii. Kila mwombaji aambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa au hati halisi ya kiapo;
- iv. Mwombaji aambatishe maelezo binafsi (CV) yakionesha namba yake ya simu na anuani yake ya makazi;
- v. Mwombaji aambatishe picha zake ndogo (passport size) mbili za hivi karibuni;
- vi. Mwombaji aambatishe barua iliyosainiwa na wadhamini wake watatu, anuani zao za makazi, picha zao ndogo (passport size) mbili za hivi karibuni na namba ya kitambulisho cha Taifa;

- vii. Mwombaji aambatishe barua ya utambulisho kutoka kwa Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa au Kijiji katika eneo analoishi;
- viii. Mwombaji aainishe juu ya bahasha kituo cha kazi anachoomba kupangiwa kati ya Dar Es Salaam au Dodoma na kazi anayoomba;
- ix. Tume haitahusika na gharama za usafiri na kujikimu kwa mwombaji atayeomba nje ya Mkoa anaoishi;
- x. Tume haitahusika na gharama za safari za mwombaji wakati wa kufanyiwa usaili;
- xi. Maombi yote yatumwe kwa njia ya Posta. Aidha, maombi yatakayowasilishwa kwa mkono hayatapokelewa; na
- xii. Mwombaji atakayewasilisha taarifa za kughushi atachukuliwa hatua za kisheria.


Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 10 Februari, 2024.

Barua zote za maombi zielekezwe kwa:-

Mkurugenzi wa Uchaguzi,
Tume ya Taifa ya Uchaguzi,
Uchaguzi House,
Eneo la Uwekezaji Njedengwa,
Kitalu D, Kiwanja Na. 4,
5 Barabara ya Uchaguzi,
S.L. P 358,

41107 DODOMA.

Limetolewa na:-


Kajima, R. K
MKURUGENZI WA UCHAGUZI
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI
DODOMA.

30 Januari, 2024